## HALMASHAURI YA JIJI MBEYA

## MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 22/10/2021

**KATIKA OFISI YA KITENGO CHA MANUNUZI.**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

1. Adon Hajayand - Mwenyekiti
2. Bosco Komba - Katibu
3. Eng Oswald Kasambala - Mjumbe
4. Felix Danda - Mjumbe
5. Dicley Nyato - Mjumbe

**WAALIKWA KUTOKA HALMASHAURI**

1. Triphonia Kisiga - Mwanasheria

**SEKRETARIETI**

1. Enock Maganga - Afisa Ugavi
2. Ande Mwaipape - Afisa Ugavi

**AJENDA ZA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI TAREHE 22/10/2021**

1. Kufungua kikao.
2. Kuridhia ajenda.
3. Kuthibitisha muhtasari wa tarehe 30/09/2021
4. Maombi ya kuridhia matumizi ya "Force Account" kama njia ya manunuzi katika Ujenzi wa madarasa na ofisi Shule za Sekondari kwa kutumia fedha za UVIKO 19.
5. Taarifa ya manunuzi yaliyoidhinishwa na Bodi ya zabuni kwa kutumia "Circular resolutions" robo ya kwanza kuanzia Julai-Septemba 2021
6. Mengineyo
7. Kufunga kikao

**MCC/BZ/1/22/10/2021: KUFUNGUA KIKAO.**

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe katika kikao baada ya akidi kutimia na kuomba watoe michango yao kisha alifungua kikao saa 09:10 alasiri.

**MCC/BZ/2/22/10/2021: KURIDHIA AJENDA.**

Mwenyekiti alimwomba Katibu awasilishe ajenda za kikao zitakazojadiliwa siku hiyo, katibu aliwasilisha ajenda saba (7). Mwenyekiti aliwahoji wajumbe kama wanaridhia ajenda ambapo waliridhia ajenda zote saba (7) kama ifuatavyo;

1. Kufungua kikao.
2. Kuridhia ajenda.
3. Kuthibitisha muhtasari wa tarehe 30/09/2021

4. Maombi ya kuridhia matumizi ya "Force Account" kama njia ya manunuzi katika Ujenzi wa madarasa na ofisi Shule za Sekondari kwa kutumia fedha za UVIKO 19.
5. Taarifa ya manunuzi yaliyoidhinishwa na Bodi ya zabuni kwa kutumia "Circular resolutions" robo ya kwanza kuanzia Julai-Septemba 2021
6. Mengineyo
7. Kufunga kikao

**MCC/BZ/3/22/10/2021: KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI CHA TAREHE 22/10/2021.**

Katibu aliwasilisha muhtasari wa kikao cha tarehe 30/09/2021 na mwenyekiti aliwaomba wajumbe wapiti ukurasa kwa ukurasa ili kufanyia masahihisho. Wajumbe walipitia Muhtasari na kufanya marekebisho ukurasa wa kwanza (1) kwenye ajenda ya pili neno lililoandikwa "Kridhia" badala ya kuridhia. Baada ya marekebisho hayo wajumbe walikubaliana kwa pamoja muhtasari usainiwe kwa ajili ya kumbukumbu ya ofisi.

**MCC/BZ/4/22/10/2021: MAOMBI YA KURIDHIA MATUMIZI YA "FORCE ACCOUNT" KAMA NJIA YA MANUNUZI KATIKA UJENZI WA MADARASA YA SHULE ZA SEKONDARI KWA KUTUMIA FEDHA ZA UVIKO 19.**

Katibu aliwasilisha taarifa kuwa Halmshauri ya Jiji imepokea fedha za UVIKO 19 kiasi cha Tsh 1,840,000,000/= (Bilioni moja na milioni mia nane na arobaini tu) kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 92 na ofisi 36 katika shule za Sekondari ishirini na tisa (29) Katibu alifafanua kuwa:

a) Ujenzi wa madarasa na ofisi kwa fedha za UVIKO 19 yanatarajiwa kujengwa katika shule zifuatazo:

| NA | Jina la Shule | Idadi ya vyumba vya madarasa | Idadi ya Ofisi |
|---|---|---|---|
| 1 | Shule ya Sekondari Sinde | 4 | 1 |
| 2 | Shule ya Sekondari Ihanga | 8 | 2 |
| 3 | Shule ya Sekondari Nzondahaki | 2 | 1 |
| 4 | Shule ya Sekondari Uyole | 2 | 1 |
| 5 | Shule ya Sekondari Mwasenkwa | 2 | 1 |
| 6 | Shule ya Sekondari Mwakibete | 2 | 1 |
| 7 | Shule ya Sekondari Mbeya | 2 | 1 |
| 8 | Shule ya Sekondari Legico | 2 | 1 |
| 9 | Shule ya Sekondari Kalobe | 2 | 1 |
| 10 | Shule ya Sekondari Maziwa | 2 | 1 |
| 11 | Shule ya Sekondari Lupeta | 5 | 2 |
| 12 | Shule ya Sekondari Mwasanga | 3 | 1 |
| 13 | Shule ya Sekondari Samora Machel | 2 | 1 |
| 14 | Shule ya Sekondari Iyela | 10 | 4 |
| 15 | Shule ya Sekondari Nsenga | 2 | 1 |
| 16 | Shule ya Sekondari Iyunga | 2 | 1 |
| 17 | Shule ya Sekondari Iwambi | 3 | 1 |
| 18 | Shule ya Sekondari Itiji | 2 | 1 |
| 19 | Shule ya Sekondari Itezi | 6 | 2 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 20 | Shule ya Sekondari Stella farm | 2 | 1 |
| 21 | Shule ya Sekondari Isyesye | 2 | 1 |
| 22 | Shule ya Sekondari Wigamba | 2 | - |
| 23 | Shule ya Sekondari Ilomba | 5 | 2 |
| 24 | Shule ya Sekondari Lyoto | 4 | 1 |
| 25 | Shule ya Sekondari Mponja | 2 | 1 |
| 26 | Shule ya Sekondari Iganzo | 6 | 2 |
| 27 | Shule ya Sekondari Hayombo | 2 | 1 |
| 28 | Shule ya Sekondari Iduda | 2 | 1 |
| 29 | Shule ya Sekondari Forest | 2 | 1 |
| | Jumla | 92 | 36 |

Katibu aliwaeleza wajumbe kuwa ili kufanikisha ujenzi wa miradi hiyo kwa wakati na kwa ufanisi, kitengo cha manunuzi kinapendekeza matumizi ya "Force Account" kama njia ya manunuzi itakayotumika kwa mujibu wa kanuni ya 167 ya ununuzi wa umma 2013 yenye marekebisho ya mwaka 2016 na vilevile kutumia mwongozo wa "Force Account" uliotolewa na mamlaka ya ununuzi wa umma PPRA wa tarehe .......
"Force Account" ni njia ya ununuzi itakayotumika kwenye ujenzi ambao unatekelezwa na Taasisi nunuzi kwa kutumia wataalam na vifaa vyake au kwa kukodi na kutumia mafundi wengine- Hired labours au kwa kushirikisha Taasisi za Umma.

Faida za matumizi ya "Force Account" ni pamoja na;

i. Kupungua gharama za ujenzi
ii. Kuimarisha uwazi na uwajibikaji
iii. Muda wa Ujenzi utakuwa mfupi
iv. Jamii itashirikishwa na hivyo kujua mradi utakavyotekelezwa
v. Inaongeza kuaminiana
vi. Kuwepo na usimamizi wa karibu na
vii. Jamii kuimiliki Miradi na hivyo kuwepo uendelezi wa mradi

Aliwaeleza wajumbe kuwa katika kutekeleza miradi hiyo utatumika mwongozo wa matumizi ya "Force Account" wa ujenzi wa madarasa shule za sekondari kwa kutumia fedha za UVIKO 19. Kama ilivyoelekezwa na mamlaka ya usimamizi ya manunuzi ya umma ambapo zitaundwa kamati mbili zitakazosimamia ujenzi huo kama ifuatavyo:

i. Kamati ya Utekelezaji
ii. Kamati ya mapokezi

Katibu aliwaeleza wajumbe kuwa hoja hii inawasilishwa kwa mujibu wa kanuni namba 149 ya manunuzi ya umma 2013 yenye marekebisho yake ya mwaka 2016,Nukuu.. "Subject to the prior approval, in writing, of the tender board, other methods of procurement may be used where it is established that such methods may have due regard for transparency, economy and efficiency in the implementation of project" kwa msingi huo vifaa na huduma zitakuwa zinanunuliwa na kwa taratibu husika za manunuzi kifadhiwa na kutolewa kwa mafundi kwa taratibu za stoo

Wajumbe wa Bodi ya wazabuni waliipoka taarifa hii wakaijadili nakuona kuwa ni vema njia hiyo ya manunuzi ikatumika kwani imekuwa na ufanisi mzuri katika kutekeleza miradi ya serikali kwa gharama nafuu na miradi mingi kwisha kwa wakati na kuazimia kuwa:

AZIMIO 2
Ujenzi wa madarasa shule za sekondari kwa kutumia fedha za UVIKO 19 ufanyike kwa njia ya "Force Account" kama njia ya manunuzi na kwamba mwongozo wa matumizi ya njia hiyo kama ulivyotolewa na mamlaka ya kusimamia manunuzi ya umma uzingatiwe wakati wa utekelezaji na taarifa ya utekelezaji iwasilishwe kwenye kikao kijacho.

**MCC/BZ/5/22/10/2021: TAARIFA YA MANUNUZI YALIYOIDHINISHWA NA BODI YA ZABUNI KWA KUTUMIA "CIRCULAR RESOLUTION" ROBO YA KWANZA KUANZIA JULAI – SEPTEMBA 2021.**
Mwenyekiti alimwomba katibu kuwasilisha taarifa ya manunuzi yaliyopitishwa na Bodi ya zabuni kwa kupitia "Circular resolutions" kwa robo ya kwanza 2021/2022. Katibu aliwasilisha taarifa hiyo kama ifuatayo;
Katibu akiwasilisha taarifa hiyo alisema katika kutekeleza mpango wa manunuzi kitengo cha manunuzi kimefanya manunuzi ya vifaa na Huduma vyenye jumla ya Tshs 160,799,358 (million mia moja sitini laki saba tisini na tisa mia tatu hamsin na nane tuu) kwa ajili ya matumizi ya ofisi. Manunuzi hayo yaliidhinishwa kwa kutumia "circular resolution" kwa mujibu wa kanuni ya 58 ya manunuzi ya umma 2013 na marekebisho yake ya mwaka 2016 kama ifuatavyo;

| NA | MAELEZO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Shajala | 20,087,000 |
| 2 | Vilainishi na vipuri na matairi kwa ajili ya matengenezo ya magari na mitambo | 39,258,600 |
| 3 | Mafuta | 54,047,758 |
| 4 | Ununuzi wa huduma mbalimbali | 10,211,500 |
| 5 | Ununuzi wa vifaa vya ofisi | 14,010,000 |
| 6 | Ununuzi wa vifaa vya usafi na ujenzi | 23,184,500 |
| | Jumla | 160,799,358 |

Katibu alieleza kuwa Halmashauri imeendelea kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo imehusisha shule za msingi na Sekondari, Zahanati na vituo vya Afya yenye thamani ya TZS 716,638,559.00 (Million mia saba kumi na sita mia sita thelathini na nane elfu mia tano hamsini na tisa tu) kama ifuatavyo;

| NA | MAELEZO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa zahanati ya Ndanyela | 39,143,247.00 |
| 2 | Manunuzi mbalimbali shule ya sekondari Mbeya | 31,251,860.00 |
| 3 | Manunuzi mbalimbali shule ya sekondari Loleza | 15,888,315.00 |
| 4 | Ujenzi wa kituo cha afya Iyela | 47,672,500.00 |
| 5 | Manunuzi mbalimbali shule ya sekondari Iyunga | 22,776,685.00 |
| 6 | Manunuzi mbalimbali shule ya sekondari Samora | 5,170,000.00 |
| 7 | Ujenzi wa madarasa mawili na manunuzi mengine katika shule ya mchepuo wa kiingereza ya Magufuri | 51,743,820.00 |
| 8 | Ujenzi wa bwalo na madarasa ya ghorofa na manunuzi mengine katika shule ya mchepuo wa | 82,074,640.00 |

| | | |
|---|---|---|
| | kiingereza ya mkapa | |
| 9 | Ujenzi wa ghorofa kwa ajili ya madarasa shule ya msingi wa kiingereza Azimio | 151,639,205.00 |
| 10 | Ujenzi wa Hospitali ya Igawilo | 176,563,100.00 |
| 11 | Upanuzi wa maabara zahanati ya Isyesye | 5,876,660.00 |
| 12 | Ujenzi wa wodi ya wazazi zahanati ya Itensa | 32,552,200.00 |
| 13 | Ujenzi wa bweni na vyoo Iduda | 36,241,240.00 |
| 14 | Manunuzi mbalimbali zahanati ya Ituha | 10,838,987.00 |
| 15 | Manunuzi mbalimbali kituo cha Afya Ruanda | 7,236,000.00 |
| | Jumla | 716,638,559.00 |

Wajumbe wa Bodi ya Zabuni walipokea taarifa hiyo na kushauri kama ifuatavyo;
i.Wajumbe walishauri wakati wa kufanya nukuu za bei zifuatwe bei za soko
ii.Makadirio ya Mhandisi yawe yanaangaliwa kabla ya kuanza mchakato wa manunuzi.
Baada ya kujadili taarifa hiyo kwa kina wajumbe wa Bodi ya Zabuni waliridhia taarifa.

**MCC/BZ/6/22/10/2021: MENGINEYO.**
Mwenyekiti aliwauliza wajumbe kama wanamengineyo, wajumbe hawakuwa na mengineyo.

**MCC/BZ/23/22/10/2021: KUFUNGA KIKAO.**
Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao na kumsisitiza katibu afuatilie suala lao la posho, kisha alifunga kikao saa 1.15 jioni.

**Muhtasari umethibitishwa na;**

**Adon Hajayand**
Mwenyekiti wa Bodi ya Zabuni

**Bosco Komba**
Katibu wa Bodi ya Zabuni

Tarehe
21/01/022